Diaspora Council of Tanzanians in America

Jumatatu 26 Oktoba, 2020

MSIMAMO RASMI WA DICOTA: MCHAKATO WA HADHI MAALUM NA URAIA PACHA

Ndugu wanaDICOTA na wanaDiaspora waTanzania wote waishio Marekani:

Mnamo tarehe 29 Septemba, 2020, Uongozi wa DICOTA uliamua kuunda kikosi kazi cha kujadili kwa kina mchakato wa hadhi maalumu na uraia pacha, kufuatia maombi ya wanaDICOTA kufahamu msimamo rasmi wa DICOTA kuhusu mchakato huu. Ikumbukwe kuwa mwaka 2014, baada ya juhudi na mchakato mrefu wa kupigania uraia pacha, DICOTA ilipeleka mwakilishi wetu Ndg. Kadari Singo kushiriki kwenye bunge maalum la Katiba. Kwenye mchakato huo wa bunge la Katiba, badala ya uraia pacha hoja ya hadhi maalum ya watu wenye asili au nasaba ya Tanzania ilipendekezwa na kupitishwa kwenye rasimu ya Katiba.

Ndugu wanaDICOTA, mtakumbuka kuwa juma zima kabla ya tarehe 29 Septemba 2020 kulikuwa na majadiliano mfululizo kuhusu uraia pacha na hadhi maalumu kwenye jukwaa la DICOTA Village. Ili kuongeza ufanisi wa majadiliano hayo, ilishauriwa kuunda kikosi kazi kwa yeyote ambaye angependa kujadili hoja zao kwa kina na kuchangia msimamo rasmi wa DICOTA. Kati ya wanaDICOTA 109, walio pia wadau wa jukwaa la DICOTA Village, wajumbe 11 waliojitokeza kujiunga na kikosi kazi, ni kama ifuatavyo:

1. Ndg. Agnetta Kamugisha
2. Dkt. Angela Lyimo
3. Ndg. Alexander Maira
4. Ndg. Aloyce Assenga
5. Dkt. Anicetus Temba
6. Ndg. Asha Nyang'anyi (Mwenyekiti Bodi ya Wadhamini, DICOTA)
7. Dkt. Filipo Lubua (Mwenyekiti, vikao vya Kikosi Kazi)
8. Dkt. Frank Minja (Rais wa DICOTA)
9. Ndg. Geoffrey Lepana
10. Dkt. Kadeghe Fue (Katibu, vikao vya Kikosi Kazi)
11. Ndg. Sylvester Mwingira

Ndugu wanaDICOTA, wanaKikosi kazi walijadili kwa weledi na kwa kina hoja nne za msingi ili kufikia msimamo rasmi wa DICOTA katika mchakato wa hadhi maalum na uraia pacha, kwa maslahi ya wanaDiaspora waTanzania wote waishio Marekani.

Ndugu wanaDiaspora, kikosi kazi kilijadili hoja nne zifuatavyo za msingi kwa kina ili kufahamu **FAIDA na HASARA** za kila hoja;

1. **Kupigania Hadhi Maalum pekee**
    a. Faida
        i. Mchakato wake umekwisha anza ndani ya Serikali ya Muungano

ii. Zanzibar wameshapitisha sheria na sera ya Diaspora kurasimisha hadhi maalum kwa waZanzibari, hivyo itakuwa rahisi kwa Serikali ya Muungano kufanyia kazi sera ya Diaspora kwa nchi nzima
iii. Serikali imeonyesha nia ya kufanyia kazi hadhi maalum kwa wepesi zaidi

b. Hasara
i. Huu sio uraia kamili na huenda baadhi tu ya haki zikatolewa kwa wanaDiaspora wenye uraia wa nchi nyingine, mfano haki ya kumiliki ardhi, haki ya kurithisha ardhi, haki ya kufanya biashara kama waTanzania wengine na haki ya kutambuliwa kama waTanzania wakiwa ndani ya mipaka ya Tanzania na haki nyinginezo zitakazopendekezwa.

2. Kupigania Hadhi Maalum kisha Uraia Pacha

a. Faida
i. WanaDiaspora watapigania Hadhi maalum na Uraia pacha, lakini wataanza kwanza na Hadhi Maalum kisha Uraia pacha, kwa kuwa mchakato wa Hadhi maalum umeshaanza kama iliivyoanishwa 1a(i).
ii. Hii inatoa fursa kwa wanaDiaspora wanaopenda Uraia Pacha Zaidi kuendelea kuupigania baada ya kupewa Hadhi maalum.

b. Hasara
i. Itachukua mchakato mrefu na muda zaidi kuweza kufanikisha vyote
ii. Serikali inaweza isielewe kwanini wanaDiaspora endapo wakipewa Hadhi maalum bado pia watataka Uraia Pacha.
iii. Mchakato huu huenda ukawa na changamoto zaidi za kisheria.

3. Kupigania Uraia Pacha Pekee

a. Faida
i. Inakubalika na kupendwa na wanaDiaspora kwa kuwa ni haki ya kuzaliwa kama waTanzania, na uTaifa haubadiliki kama ulivyo uraia.
ii. Uraia pacha huu utahusisha waTanzania pekee, yaani wenye haki ya uraia kwa kurithishwa (by descent) au kwa kuzaliwa (by birth), hivyo kukuza uTaifa kwa wananchi.
iii. Inawajengea wanaDiaspora uhakika wa haki zao zote kama Raia wa Tanzania, na hivyo kuweka uzalendo mbele na kushiriki kuijenga nchi yao kwa nguvu kubwa zaidi.

b. Hasara
i. Hoja ya Uraia Pacha imeibua utata mkubwa miongoni mwa viongozi wa serikali, wabunge na raia wengi kwa kudhani itanufaisha wageni zaidi.
ii. Kuna uwezekano mkubwa Tanzania haijawa tayari kisiasa kuruhusu Uraia Pacha

Diaspora Council of Tanzanians in America

4. **Kupigania muunganiko wa Uraia Pacha na Hadhi Maalum yaani Uraia wa Hadhi maalum (Citizenship by Special Status).**
    a. Faida
        i. Ni uraia kwa mtu mwenye sifa ya uraia kwa kuzaliwa (by birth) au kwa kurithi (by descent) na wazazi waTanzania lakini akamua kuchukua uraia wa nchi nyingine.
        ii. Hakuna raia wa nchi nyingine ambaye hana sifa ya uraia wa kuzaliwa au uraia wa kurithi, ataweza kupewa uraia huu.
        iii. Huu ni uraia kama uraia mwingine wa Tanzania kwa hiyo kupata haki zote muhimu kama raia wengine
    b. Hasara
        i. Uraia huu wa "muunganiko" ni mgeni miongoni mwa wajumbe wa kikosi kazi, hivyo huenda usipokelewe vizuri na wanaDiaspora.
        ii. Uraia huu huenda ukawa na mapungufu ya haki baadhi, kama haki za kuwa kiongozi wa umma au kugombea nafasi za kisiasa – haki ambazo hazikupewa kipaumbele na wanaDiaspora kwenye utafiti wa DICOTA.

Ndugu wanaDiaspora, baada ya kujadili kwa kina hoja hizi nne za msingi, pamoja na faida na hasara zake; kikosi kazi kiliamua kupiga kura kuchagua hoja mojawapo. Hoja ya pili: **kupigania hadhi maalum kisha uraia pacha** ilipitishwa kwa kura nyingi kuliko hoja nyingine. Hivyo basi, msimamo rasmi wa DICOTA ni **kupigania hadhi maalum kisha uraia pacha**.

Ndugu wanaDiaspora, pamoja na uamuzi huu wanakikosi kazi walikiri pengo kubwa la uelewa wa pamoja miongoni mwa wanaDiaspora kuhusu hoja hizi nne za msingi, na hivyo basi kuna uhitaji mkubwa sana wa kuelimishana sisi wanaDICOTA, tukishirikiana na wanaDiaspora waTanzania wote waishio Marekani.

Ndugu wanaDiaspora, hili tamko rasmi ni mwendelezo wa mchakato wa hadhi maalum na hatimaye kufikia uraia pacha. WanaDICOTA na wanaDiaspora waTanzania wote waishio Marekani mnahimizwa kujiunga na kusaidia juhudi za DICOTA pamoja na vikosi kazi kwa kadri ya uwezo wenu, ili kufanikisha maslahi yetu na kwa vizazi yetu.

Ndugu wanaDiaspora, Asanteni sana kwa ushirikiano na usikivu wenu.

Kwa niaba ya Kikosi Kazi na Uongozi wa DICOTA

Dkt. Frank Minja
Rais, DICOTA

Ndg. Asha Nyang'anyi
Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, DICOTA